Imani Ya Mariamu

. . .leso hizi zinazowakilisha wagonjwa na wanaoteseka kote nchini. Wewe unabaki Mungu, wala huwezi kukosa kujibu maombi yanapofanywa kwa uaminifu na imani. Tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utawabariki watu hawa, jalia wapone kutokana na magonjwa yao na mateso. Jalia leso hizi ziwe ishara za mkutano huu usiku wa leo, na imani tunayokutolea Wewe kutoka kwenye vilindi vya moyo wetu. Tujalie, Bwana. Jalia kila nguvu za magonjwa yanayowashikilia watu, jalia yaondoke mara leso hiyo itakapougusa mwili wao. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

2 Mnaweza kuketi. (Asante, Ndugu du Plessis.) Nilikuwa tu nimechelewa kidogo, hali mbaya ya hospitali, mtu, mahututi sana, aliletwa tu hapa ambaye asingeweza kungojea, ilibidi tu atolewe moja kwa moja kutoka hospitalini, na ni mahututi sana, sana, sana. Nikamwambia huyo mtu, "Unaamini, bwana?"

3 Akasema, "Nilikuwa nimestarehe hospitalini, lakini nimekuwa nikikungojea kwa uchungu." Ninaamini tu ya kwamba Mungu atamponya na kumruhusu awe mzima, aende nyumbani awe mzima sasa, kwa ajili ya utukufu Wake.

4 Usiku wa leo ninataka tu kuchukua dakika chache tu za wakati, kupata tu hisia za mkutano. Ndipo tutawaombea wagonjwa, tufanyize mstari wa maombi moja kwa moja kama tulivyosema tungefanya, ahadi.

5 Na sasa, kesho asubuhi saa mbili ni kiamshakinywa cha Wafanyabiashara. Nafikiri hiyo ni kweli, Ndugu Shakarian. Hakika nina furaha kuwa na Ndugu Shakarian hapa pamoja nasi usiku wa leo jukwaani. Ndugu Miner Arganbright mahali fulani mkutanoni, na pia Ndugu Bonham, marafiki zangu wazuri kweli ambao wamesafiri karibu sehemu ya, sehemu kubwa ya ulimwengu pamoja nami mikutanoni.

6 Na kesho asubuhi kutakuwa na Wafanyabiashara, tawi la Wafanyabiashara wa Full Gospel litakaloanzishwa hapa katika mji wenu. Nafikiri ni rasilimali. Nami nafikiri ni. . .Mimi mwenyewe nimefurahi sana juu yake, kujua ya kwamba itakuwa ni huduma nyingine ya Ufalme wa Mungu, huduma nyingine ya kusaidia. Nao wafanyabiashara, kama nilivyosema jana usiku, sisi—sisi wahudumu. . .

7 Jinsi karibu si—sikuwahi hata kumjua Ndugu Shores, mpaka kwenye mkutano huu, nasi tunakuja pamoja na kuzungumza, tuna mambo shirika, ni Ufalme wa Mungu. Nasi tunapenda kukusanyika pamoja na kuzungumza mambo haya. Wahudumu wana ushirika, sisi ni wafuasi wa madhehebu mbalimbali na

kadhalika, ambalo hilo halitusumbui. Tuna furaha kwamba neema ya Mungu huangalia juu ya hayo yote, na kuninii tu. . .

8 Lakini basi wafanyabiashara, baadhi yao huingia, na mmoja ni makanika, huyo mwingine ana biashara ya magari, mwingine biashara ya maziwa, hawaambiani, "Vema, wewe si muuza maziwa, huko ndani yake." Wanafanya tu ushirika wao kwa wao. Mnaona? Nami nafikiri wana mambo shirika, na ni vizuri kwao kuyazungumzia. Hawaji kamwe, hawaji sasa kupachukua mahali pa Kanisa. Wanakuja tu kuongezea Kanisani, kulisaidia Kanisa katika haya mapambano makuu. Bwana na abariki, ndilo ombi langu.

9 Ndugu Williams alitangaza hivi majuzi usiku ya kwamba hawakuwa na nafasi kwa ajili ya kina mama. Ninasikitika kuhusu hilo, kwa sababu kina mama kweli huhudhuria mikutano, mwajua. Lakini nawaambieni ule ufuatao. . . Basi nawaambia, ya kwamba na—na—napenda kuja Phoenix pamoja na wahudumu, na halafu hili litafanya jambo lingine linalonibidi kulijia Phoenix, kwa ajili ya kiamshakinywa hiki mara moja moja. Nami ninazungumza kwa niaba yao, kila mahali. Halafu ninyi kina mama ni, shukeni mje moja kwa moja basi, nasi tutatumbukiza tu mikono yetu kwenye gudulia la asali, mwajua, na kuwa na wakati mzuri katika Bwana.

10 Sasa, kwa kuwa kunachelewa, nataka tu dakika chache, kwa sababu nina hakika kwamba ni vigumu kufundisha nyuma ya David du Plessis. Naye tayari, hapana shaka, amewapa ujumbe wa kutosha wa Injili usiku wa leo ambao ungeridhisha ku—kusanyiko zima. Lakini ili tu nipate hisia ya umati, ninataka kutoa maneno machache tu ya kusoma kutoka katika Luka Mtakatifu mlango wa kwanza, kama mngetaka kufungua mlango huu, ninyi mnaoiandika milango.

11 Halafu kesho usiku, Bwana akipenda, tunataka ibada tatu za uponyaji, kesho. . . usiku wa leo, kesho usiku, na Jumapili usiku, mpaka tutakapoumaliza umati wote kwenye mistari. Wala hatuwezi kuwamaliza wote katika usiku mmoja, bali tunakusudia kufanya tuwezavyo kuwapitisha, kwa vyovyote vile, kadri ya uwezo wetu. Kwa hiyo ninyi mtuombee.

12 Na sasa, Jumapili asubuhi itakuwa kwenye kanisa lako mwenyewe ulilochagua. Nanyi wageni hapa, tafuteni moja ya makanisa haya mazuri hapa Phoenix, kanisa unalohudhuria, dhehebu lako mwenyewe. Kuna wahudumu wengi wanaohudhuria mkutano huu hapa wangefurahi kuwa pamoja nanyi kwenye ibada zao za Jumapili asubuhi.

13 Ni wahudumu wangapi waliopo hapa? Inueni mikono yenu, kote kila mahali. Ninawatakeni mwone ni wahudumu wangapi walioko humu jengoni. Angalieni hapo, hao ni wahubiri, thelathini, arobaini, labda, wameketi humu jengoni usiku wa leo. Jinsi tunavyoshukuru kwa ajili ya watu hawa wazuri wa Mungu,

na wanawake wa Mungu, wanaomwamini Bwana Yesu Kristo katika huduma ya namna hii!

14 Hebu na tuanze kusoma sasa, katika mlango wa kwanza wa Luka Mtakatifu, na kuanzia kifungu cha 35:

> *Malaika akajibu, akamwambia, Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake Aliye juu zitakufunika kama kivuli: kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa Mwana wa Mungu.*
>
> *Tena, tazama, binamu yako Elisabeti naye amechukua mimba ya mtoto mwanamume katika uzee wake: na mwezi huu ni wa sita kwake yeye aliyeitwa tasa.*
>
> *Kwa maana hakuna neno lisilowezekana kwa Mungu.*
>
> *Mariamu* akajibu *akasema, Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana; na iwe kwangu kama ulivyosema. Kisha malaika akaondoka akaenda zake.*

15 Hebu na tuombe mara nyingine tena, tafadhalini.

16 Bwana, sasa, tumeimba nyimbo usiku wa leo. Kamwe sikupata nafasi ya kuuimba pamoja na hawa watu, ila kuvumisha tu kidogo *Amini Tu*, nilipokuwa nikija mimbarani. Maombi yamefanywa, Biblia imesomwa. Bwana, nena nasi usiku wa leo kupitia Neno Lako, kuuendeleza Ujumbe ambao tayari tumeusikia. Tunaomba ya kwamba basi Roho Mtakatifu atakuja na kuingia kwenye Ujumbe usiku wa leo, naye atamleta Kristo, halisi, mioyoni mwetu.

17 Tumesikia gazetini, ambapo hao Waislamu waliwaweka watu thelathini wenye magonjwa yasiyotibika mbele ya Bw. Billy Graham na kumpa changamoto. Ee Bwana Mungu, kungali kuna Mungu anayeishi na kujibu kwa Moto. Tunakuomba Wewe, Baba wa Mbinguni, uwe pamoja na Billy Graham wakati akihudumu huko hudumani ambako ni wale tu wanaotembea kwenye njia hizo . . .

18 Mara nyingi ambapo mtumishi Wako amejaribu kuwaambia watu, "Ni sawa hapa Marekani, bali usijaribu nchi hiyo ya pepo kule, isipokuwa unajua unachozungumzia, kwa kuwa wako tayari kumpa changamoto Roho wa Mungu."

19 Bwana, Wewe ungali ni Mungu, na umethibitisha kila wakati ya kwamba Wewe ni Mungu. Wape watumishi wako ujasiri kukuamini Wewe, Bwana. Wewe ni Mungu, kama Wewe si Mungu yeye yule, basi hukuwa Mungu hata kidogo. Lakini tunajua ya kwamba Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele, wala hakuna kitu kinachoweza kukubadilisha Wewe, Wewe ni Mungu wa daima na wa milele. Nena nasi usiku wa leo, Bwana Yesu, tunapolitafakari Neno Lako. Tunaomba, katika Jina Lako, na kwa ajili Yako. Amina.

20 Ninaamini ya kwamba jua lilikuwa tayari limechomoza na lilikuwa likiangazia anga za Galilaya, likivuta harufu nzuri

ya waridi, kwa maana usiku ulikuwa mtulivu, na utamu huja hewani, naye alikuwa akishuka kwenda kando ya barabara kwenye kisima cha mjini, ambapo watu huja kuteka maji yao. Naye alipokuwa akienda zake na maskini mtungi wake mkononi mwake, alikuwa akitafakari, akiwazia juu ya siku iliyotangulia na ule ujumbe mkuu wenye nguvu ambao rabi alikuwa amehubiri, na kwenye ujumbe ambao yeye na Yusufu, mume wake mchumba, walikuwa wameuzungumzia kwenye baraza lao la mbele baada ya mlo wa adhuhuri.

21 Walipokuwa wameketi pale, wakiangalia ng'ambo ya pili ya kilima kidogo ambapo, hatimaye, maskini ile nyumba ingejengwa ambamo wataishi, kadiri walivyojua, katika jengo hili dogo . . .

22 Yusufu alikuwa seremala, naye aliipenda kazi yake, naye alipenda kufanya mambo vizuri kabisa. Na akiwa anamwamini Mungu na kujua ya kwamba kulikuwa na Mtu fulani aliyemlinda, alitaka kazi yake yote iwe sawa kabisa. Lakini loo, maskini nyumba hii ilikuwa ni maalum, ilibidi milango iwe mikamilifu kabisa, pamoja na vyu—vyumba vya faragha ndani yake, kwa sababu alikuwa amlete mwanamke mzuri kuliko wote ulimwenguni kote mle awe bibi-arusi wake.

23 Basi wakati wao, kama ilivyokuwa desturi, wangeketi huko nje na kutazama maskini hiyo nyumba, na kupanga jinsi maua ya waridi yatakavyokuwa mahali hapa padogo, nalo lango halina budi kuwa na moyo mdogo, kwa sababu walikuwa wanapendana sana. Na jinsi walivyokuwa wakipanga kufanya jambo hilo, kwa sababu Yusufu akiwa seremala, mbona, angeweza kuchukua wakati wake. Halafu basi, labda, nyuma tu ya hiyo nyumba, kungekuwa na duka la seremala, ambapo angefanya kazi yake yote ya kabati, kutengeneza milango yake, na—na vikorokoro vidogo alivyoletewa, na katika hiyo, wangepata riziki yao.

24 Na Jumapili hii, mara walipotoka, ama, Sabato, na kuketi kwenye baraza la mbele baada ya mlo wa adhuhuri, hapana shaka Yusufu ndiye aliyesema, "Huo ulikuwa ujumbe wa kuvutia sana asubuhi ya leo, Mariamu. Ninafurahi sana ninapomsikia rabi wetu akizungumza juu ya ukuu wa Yehova. Na, loo, jinsi alivyotwambia juu ya yule Mungu mkuu, mwenye nguvu aliyeshuka akaja Misri na kuwatoa watu wetu, jinsi alivyoifungua Bahari ya Shamu wakati ilipomzuia, na jinsi alivyonyesha mkate kutoka Mbinguni, akawapuliza kware kutoka kondeni, akawaongoza kwa Nguzo ya Moto usiku, na Wingu mchana.

25 "Na jinsi wana wa Israeli walivyopiga kambi chini ya Nuru hii kuu walipotembea katika Nuru, popote ilipoenda, walienda, pia, na kuwaleta salama katika nchi ya ahadi."

26 Basi huenda Mariamu alisema kitu kama hiki, "Naam, Mpenzi, lakini nataka kukuuliza jambo fulani. Ilikuwaje kwa

huyo Mungu mkuu, kwamba Yeye si mkuu leo kama alivyokuwa wakati huo? Hivi ulimwona rabi baada ya ujumbe huo mzuri sana, halafu ole, akasema, 'Hapana shaka Yehova alitupa kisogo, kwa sababu hafanyi miujiza tena'"?

Lakini Yusufu upesi akalifuatilia, na kusema, "Lakini, Mariamu, ninaamini ya kwamba Mungu ni mkuu tu na mwenye nguvu kama alivyowahi kuwa."

27 Juu ya hilo, mama yake Mariamu, Ana, hapana shaka alikuja mlangoni, na kusema, "Je, ninyi vijana mnayangojea Maandiko?" ndipo akakiweka mkononi mwa Mariamu, ambaye alimkabidhi Yusufu, Kitabu cha Isaya.

28 Yusufu akifungua hilo Gombo, akaanza kusoma, ndipo alipofikia Isaya 9:6:

> . . . *kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume: na* ninii yake. . . *uweza wa kifalme utakuwa begani mwake:* . . . *jina lake ataitwa* . . . *Mshauri*, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele.
>
> . . . *na amani* Yake na Ufalme Wake *havitakuwa na mwisho*.

29 Na hapana shaka ilikuwa ni wakati huo ambapo moyo wa Mariamu ulionywa kwa njia ya ajabu. Si ni ajabu jinsi Mungu anavyofanya mambo haya? Maandiko yanadhihirishwa. Akasema, "Yusufu?"

30 Naye akamtazama, na labda sikuzote alidfikiri alikuwa ndiye mwanamke mrembo kuliko wote aliopata kuwaona, lakini basi kulikuwa na mtazamo fulani usoni mwake ambao ulimvutia zaidi kuliko hapo awali, huku macho yake mazuri yakimtazama kama ya hua, laini, yasiyo na hatia. Nafikiri hivyo ndivyo mwanamke anavyopaswa kuonekana, asiye na hatia, laini, na mzuri.

31 Akasema, "Yusufu, nabii alikuwa akinena juu ya nini aliposema, 'Kwa ajili yetu Mtoto amezaliwa, na tumepewa mtoto Mwanamume'? Ni nani huyu Mwana na Mtoto huyu aliyekuwa akinena habari zake?"

32 Yusufu akamtazama, hapana shaka, na kusema, "Vema, mpendwa wangu, nabii alikuwa akizungumza juu ya Masihi ajaye, Tumaini la Israeli. Nawe unajua, Mariamu, ya kwamba kote katika nyakati zote tangu Musa, tumemtazamia Huyo anayekuja. Naye atakapokuja, atatukomboa kutoka katika utumwa wa hawa Warumi, kutoka katika utumwa wa dhambi zetu, nao Israeli watamjua Mungu wao, Naye atatimiza Neno Lake. Na Mariamu, mpendwa wangu, tusipomwona katika kizazi chetu, hakika Yeye atakuwa hapa katika kijacho. Lakini tutamtazamia katika kizazi chetu."

33 Usiku kucha, asingeweza kulala juu yake: "Kwa ajili yetu Mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto Mwanamume." Basi kesho yake asubuhi, alikuwa amechelewa kulala, kwa hiyo alichelewa kufika kisimani, hiyo ndiyo sababu jua lilikuwa limechomoza. Ndipo aliposhuka kwenda barabarani, ilionekana kana kwamba hakukuwa na mtu karibu, naye alikuwa akiwazia juu ya Andiko hili. Na kwa kawaida ni wakati tunapowazi-. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

34 Ninaamini ya kwamba hiyo ndiyo sababu watu hawana ushindi, na, moyoni mwao wanaopaswa kuwa nao, ni kwa sababu mawazo yao yako juu ya mambo mengine. "Jalia tafakari ya nia yangu, ya moyo wangu, ikubalike Kwako, Ee Bwana." Ninaamini kama tutatafakari juu Yake, Yeye atatukaribia.

35 Mnakumbuka ile Pasaka ya kwanza, wakati Kleopa na rafiki yake asiyetajwa jina, katika Biblia, walipokuwa wakienda zao Emau? Walikuwa wakitembea barabarani wakijadiliana juu Yake, wakitafakari juu Yake. Loo, mioyo yao ilikuwa imelemewa, kila tumaini lilionekana kana kwamba walikuwa nalo liliondolewa kwao, na hapo ndipo Mgeni alipotokea kando ya kichaka na kutembea pamoja nao. Hawakujua alikuwa ni Nani, Yeye alikuwa ni Mwanadamu tu, akatokea akitembea, akatembea pamoja nao, na kusema, "Mbona mmechoka sana? Mbona mmehuzunika sana akilini mwenu?"

36 Nao wakasema, "Kwani wewe ni Mgeni tu? Hivi hujui ya kuwa Yesu wa Nazareti, Ambaye tulimtarajia kuwa Mkombozi wa Israeli, amesulubiwa na Pilato? Na hii ni siku ya tatu, baadhi ya wanawake walisema waliona ono la Malaika."

37 Ndipo akaanzia kwenye Maandiko, akaanza kuwaelezea Maandiko, jinsi ambavyo imempasa Kristo kuteswa na kuingia katika utukufu Wake. Ndipo basi alipowaingiza chumbani na kufunga milango, Naye akafanya mwujiza, ama kitu fulani kama tu alivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwake, nao wakajua ilikuwa ni Yeye.

38 Kutafakari juu Yake, loo, laiti tusingalikuwa na mambo mengine mengi akilini mwetu! Mwajua, wakati mwingine tutakuja kanisani, tukiwazia, "Kesho sina budi kufanya *hivi*, kesho yake, sina budi kufanya *hivi*." Tunapokuja kanisani, tunapaswa kuweka kando kila wazo na kila kitu cha ulimwengu, na kuingia katika ushirika pamoja na Kristo na kuabudu, tukitafakari, tukiabudu mioyoni mwetu, na kumpa Yeye nyimbo na sifa, tukiwaza juu ya wema Wake, na kile anachomaanisha kwetu, tukiabudu katika Roho, tukiimba nyimbo za kiroho, tukiimba nyimbo tamu moyoni mwetu. Hata Biblia ilisema, "Kama kuna wowote wanaoteseka, na waimbe zaburi." Furahi, kuwa ukitafakari, daima ukimtarajia Mungu wakati wowote kukutokea.

39 Unafanya hivyo sasa hivi tu kabla ya ibada hii ya uponyaji? Ninyi watu mlio na kadi za maombi, mnaoungojea mstari, hivi mnawazia, “Katika dakika chache tu zaidi, na mateso yangu yote yatakwisha”?

40 Hivi mnawazia, “Loo, sijui, huenda asiite kadi yangu. Mimi . . . Huenda ikawa . . . ”?

41 Loo, usifanye hivyo. Kumbuka tu, liweke tu niani mwako, “Itakuwa tu dakika chache sasa,” nawe utatimiza masharti ambayo Mungu alisema utimize. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Mweke niani mwako.

42 Naye alikuwa akiwazia juu ya Maandiko, Andiko hilo lilikuwa likithibitishwa kwake, “Mtoto amezaliwa, tumepewa Mwana.” Na yapata wakati huo, aliona kitu fulani kikimulika mbele ya maskini huyo bikira, na Nuru, hapana shaka niani mwangu, kama ile Nguzo ya Moto, na pale alisimama Malaika, Gabrieli mwenye nguvu, yeye ni mjumbe kwa Wayahudi. Kumbukeni, Gabrieli alitangaza kuja kwa kwanza kwa Kristo, Malaika Gabrieli atatangaza kuja kwa pili kwa Kristo, Biblia ilisema hivyo.

43 Sasa, hapo, ilimtisha maskini mama huyo, naye akamtazama, naye akasema, “Salamu, Mariamu, umebarikiwa miongoni mwa wanawake. Umepewa neema sana na Mungu, kwa maana Mungu yu pamoja nawe.” Naye akawaambia yale yatakayotukia, ya kwamba atazaa Mtoto, nao watamwita Jina Lake YESU, kwa kuwa Yeye angewaokoa watu na dhambi.

44 Sasa alikuwa na haki ya kujua ya kwamba huyo alikuwa ndiye mjumbe wa kweli. Jambo la kwanza, alikuwa ni Malaika aliyesimama pale, jambo lingine, alimwambia yeye alikuwa ni nani, Mariamu. Alijua hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Mungu kote katika nyakati. Akamwangalia, naye akasema, “Mambo haya yanawezekanaje, kwa kuwa simjui mwanamume?”

Naye akasema, “Roho Mtakatifu atakujilia juu yako.”

45 Kabla miujiza haijatendeka, Roho Mtakatifu hana budi kuja. Hiyo ndiyo shida ulimwenguni leo, wanakana nguvu za Roho Mtakatifu. Hiyo ndiyo sababu watu hawawezi kuamini katika uponyaji wa Kiungu, wanamkana Roho Mtakatifu yeye yule aletaye uponyaji wa Kiungu.

46 “Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, naye Aliye Juu atakutia uvuli. Na Kitu hicho Kitakatifu kitakachozaliwa kwako kitaitwa Mwana wa Mungu. Hivyo ndivyo Yeye anavyokuja, huna haja ya kumjua mwanamume yeyote, Mungu atafanya jambo hili. Kwa maana kwa Mungu, hakuna lisilowezekana.”

47 Loo, kile maskini mama huyo ilimbidi kuamini! Ilimbidi kuamini jambo ambalo lilikuwa haliwezekani, ilimbidi kuamini jambo ambalo halikuwahi kutukia kamwe.

48 Hana, wakati alipoambiwa na kuhani, “Bwana na akupe haja yako,” mbona, alienda nyumbani, katika miezi tisa akamleta mtoto. Hilo lilikuwa zuri sana. Lakini, na Elisabeti vivyo hivyo, kama alivyosema, “Elisabeti binamu yako, ambaye aliitwa tasa, tayari ana mimba ya miezi sita.” Naye akamwambia kwamba kwa Mungu, hakuna lisilowezekana.

49 Naye akasema, “Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana, na iwe kwangu kulingana na Neno lako.” Kile kilichombidi kuamini, jambo ambalo halikuwa limewahi kutendeka kamwe.

50 Zakaria kuhani, mume wa binamu yake, alimtilia shaka Malaika yuyo huyo wakati aliposema baada ya siku za huduma hekaluni, angeenda nyumbani na kuishi na mke wake, Elisabeti, naye angemzaa mwana. Naye akasema, “Mimi ni mzee sana, haiwezekani.” Loo, alitilia shaka tu jambo hilo, naye alikuwa na Ibrahimu na Sara wa kuwaangalia, alikuwa na Hana hekaluni, na Eli mumewe wa kuwawazia, bali huyo kuhani mgumu alitilia shaka Neno la Mungu.

51 Lakini kama Ndugu Shakarian alivyosema hivi majuzi kule kisiwani, nilipomwona mama mkwe wangu akifa siku tano kabla halijatukia, naye shemeji yangu akitokwa na damu, na akitema damu kutoka kinywani mwake, ikifoka tu kutoka kinywani mwake, Ndugu Sonmore akasema, ‘Hebu tuingie ndani tukaombe, kwamba jambo hili lisitendeke.”

Nikasema, “Haitafaa kitu hata kidogo. Mungu tayari amesema jambo hilo, halina budi kutukia.”

52 Mungu, anaposema jambo lolote, haiwezekani lisitendeke. Kwa hiyo, Mungu anaposema katika Vitabu, “Mambo yote yanawezekana kwao waaminio,” halina budi kutukia. Hakuna njia ya kulielezea vinginevyo. Unaweza kuamini Mungu atatimiza kila ahadi aliyotoa.

53 Basi wakati. . .Hakungojea kamwe, maskini Mariamu hakungojea. Sasa, ilimbidi kuamini jambo ambalo halikuwa limetukia kamwe. Lakini angalieni maskini moyo wake wa kitoto, nitamwazia kuwa ni msichana tu mwenye umri wa miaka kama kumi na minane, ishirini, kamwe hakuchukua wazo la pili. Mara alipoona na kujua huyo alikuwa ni Malaika wa Bwana, aliyejua mambo haya, na kumwambia kulingana kabisa na Maandiko aliyokuwa akiwazia, na kumwambia jina lake, alijua mjumbe huyo alitoka kwa Mungu. Nayo Maandiko aliyokuwa akiyawazia yalithibitishwa papo hapo kwake.

54 “Mariamu, Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na Mwenyezi atakutia uvuli. Na Kitu hicho Kitakatifu kitakachozaliwa hakitakuwa cha mwanadamu, bali Yeye ataitwa Mwana wa Mungu.”

55 Akaitupa maskini mikono yake juu, huku machozi yakitiririka kutoka kwenye macho hayo mazuri, kasema, “Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana; na iwe kwangu sawasawa na Neno Lako.”

56 Hakungojea mpaka alipokuwa na hakika ya jambo hili, hakungojea mpaka alipohisi uhai, ama namna fulani ya msisimko kuthibitisha ya kwamba ni mja mzito, aliamini tu Neno lake, na hilo lilitosha.

57 Hivyo ndivyo Mungu anavyokutaka ufanye usiku wa leo, si kungojea mpaka ujisikie vizuri zaidi, si kungoja mpaka uweze kuusogeza mkono wako vizuri zaidi, ama kupiga hatua nzuri, si kungoja mpaka daktari aseme unapata nafuu, bali chukua Neno la Mungu na uanze kuliamini. Hiyo ndiyo njia pekee ya kumpendeza Yeye, liamini Neno Lake. Hivyo ndivyo miujiza inavyofanywa. Wakati Neno la Mungu linapoaminiwa, yasiyowezekana yanafanywa halisi, wakati Neno la Mungu linapoaminiwa, sio kuhojiwa. Lichukue tu kutoka niani mwako.

58 “Tazama, mjakazi wa Bwana.” Ndio sababu alilifurahia sana, asingeweza kusimama kimya, hata hakuna kitu kilichokuwa kimejitokeza bado, bali alijua yangetukia, kwa sababu Mungu alisema hivyo.

59 Kama Kristo alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya,” amini Neno Lake. Usishuku chochote, endelea tu kuamini, itakuwa sawa. Mungu aliahidi jambo hilo, Mungu atalitimiza, Mungu huliangalia Neno Lake apate kulitimiza na kujibu maombi.

60 Ndipo akaanza kwenda zake. Alisikia habari njema za binamu yake, Elisabeti, mwanamke mkongwe, yapata umri wa miaka sitini na mitano, sabini, mumewe mwenye umri ule ule, yapata umri wa miaka sabini ama sabini na mitano, naye alikuwa amechukua mimba katika uzee wake, kwa sababu alikuwa ameamini Mungu angempa mtoto.

61 Ilikuwa ni heshima wakati huo kupata mtoto, ni fedheha sasa. Afadhali wanunue mbwa mdogo, wampe upendo wa mtoto. Si ajabu tuna uhalifu wa vijana, tuna mama wanaopenda mbwa. Hiyo ni, loo, ni aibu! Lakini ilikuwa ni heshima wakati huo, na aibu kwa mwanamke kutopata mtoto.

62 Lakini maskini Mariamu akashika safari, kutoka Nazareti, hadi kwenye vilima vya Uyahudi, akapandia ile njia mbovu (nadhani, Ndugu Arganbright, ulisafiria njia hiyo majuma machache yaliyopita.), akapanda kilima hicho kuingia Uyahudi kukutana na binamu yake, kufurahia ushirika pamoja, kwa sababu Mungu alikuwa amewatia uvuli wote wawili.

63 “Ni majaliwa ya jinsi gani kwa ndugu kuishi pamoja katika umoja! Ni kama mafuta ya kutia yaliyokuwa kwenye ndevu za Haruni, yaliyoshuka hadi kwenye upindo wa vazi lake.” Wakati

watu pamoja wanapoweza kukubaliana kwamba Mungu angali ni Mungu, Mungu ni mkuu tu kama alivyowahi kuwa, nao wanaweza kukusanyika pamoja na kumwabudu Mungu katika Roho!

64 Mariamu alitaka ushirika. Hakuna haja ya kushuka kwenda kwenye sinagogi, kwa sababu hawakuliamini, alimwendea mtu fulani aliyekuwa na tukio kama alilokuwa nalo, naye alienda huko kufanya ushirika. Kwa hiyo, alishika njia akaenda kwa mtu aliyeamini Mungu alikuwa angali ni mkuu tu kama alivyowahi kuwa.

65 Hiyo ndiyo sababu tunafanya ushirika huu wa Wafanyabiashara Wakristo asubuhi, ambapo wafanyabiashara wanaweza kuabudu pamoja katika msingi mmoja, wakiamini ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Hiyo ndiyo sababu tuna makanisa kote katika mji huu, na kote ulimwenguni, wanaohubiri utajiri wa Kristo usiotafutika, kwa sababu tuna ushirika pamoja. Tumeketi katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, Roho Mtakatifu akija juu yetu, na kututia uvuli, akitutia nguvu kwa karama, na ishara, na maajabu, na miujiza. Mbona, ndicho kitu kilicho karibu sana na Mbingu kilichoko duniani!

66 Hapo akashika njia kuhudhuria ushirika huu; moyo huutamani. Huyo juu ya vilima, ninaweza kumwona akienda, maskini mashavu yake yakiona haya na hayo macho madogo yakimetameta, wakati akiwazia, “Nitamficha Yusufu siri hii. Siwezi kabisa kungojea, sina budi kwenda.”

67 Naye huyo akapanda vilimani, akapanda akaingia Uyahudi, huko juu kwenye nyumba ya binamu yake. Naye Mariamu, kabla hajafika nyumbani . . . Elisabeti, binamu yake, alikuwa amejificha, kwa sababu alikuwa amechoka sana, kwa sababu mtoto Yohana, katika tumbo la uzazi la mamaye, alikuwa na miezi sita wala hakuna uhai uliokuwa umejionyesha bado. Sasa, hilo kwa jumla si la kawaida, si utaratibu hasa wa kawaida. Uhai hutokea katika miezi mitatu au minne, na hii ni miezi sita, naye alikuwa na wasiwasi kidogo juu yake.

68 Ninaweza kumwona ameketi nyuma chumbani, naye huyo hapo ameketi akiomba kitu kama hiki: “Mungu, nimengojea miaka hii yote, nami niliamini moyoni mwangu kwamba jambo fulani lilikuwa karibu kutukia. Huyo hapo mume wangu ameketi huko nje, bubu, hawezi kuzungumza, naye anaendelea kuandika ubaoni, na kusema, ‘Nilimwona Malaika! Nilimwona Malaika! Malaika alinena nami kwenye mkono wa kuume wa madhabahu, jambo fulani kuu linaenda kutukia!’”

69 Ndipo kwa ghafla, akaona ya kwamba alikuwa mja mzito. Lakini yeye . . . Mtoto huyo alikua, lakini hakuwa na uhai, hakuna msogeo wa misuli hata kidogo, miezi sita, sio kawaida kabisa. Ndipo akachungulia dirishani, akamwona Mariamu

akija, meno yake yakimetameta kama lulu, na macho yake yakimetameta tu kwa furaha.

Ndipo akasema, "Ninapaswa kumjua mtoto huyo."

70 Naye alikuwa amejifunika joho lake, akikimbia kwa nguvu alivyoweza. Zakaria alisimama uani, akasema, "Loo, salamu! Ninajua wewe ni nani, mimi . . . wewe ni binti ya Anna, wewe ni binti ya Anna."

"Naam, ni mimi huyo."

71 Ndipo Elisabeti akatoka mbio, alikuwa ameketi mle ndani akishona vijibuti kwa ajili ya mtoto mchanga, *kwa namna fulani*, aliamini huko chini kabisa moyoni mwake ya kwamba Mungu asingempungukia. Haidhuru . . .

72 Labda umeketi mgonjwa, labda umejaribu kumtumikia Mungu, nawe umeketi mgonjwa usiku wa leo, lakini huko chini kabisa moyoni mwako, *kitu fulani* kinajiandaa. Loo, sijui kama huyu mtu hapa kwenye kiti cha magurudumu, kama yuko tayari, akipata, akiwazia chini moyoni mwake, "Huu ndio ule usiku! Kamwe haitanilazimu kutumia hiki tena."

73 Nashangaa kama mama huyu aliyeketi hapa, na huyo aliye nyuma yake, wanawazia jambo lile lile? Kama wengine, mama mwingine aliyeketi kule nyuma, mnakumbuka ya kwamba mambo yote hufanya kazi pamoja kwa manufaa ya wale wampendao Mungu? Mungu anajaribu kukufanyia jambo fulani.

74 Basi akaweka chini maskini vijibuti, kisha akakimbia uani. Ndipo akamshika Mariamu shingoni, akaanza kumkumbatia na kumbusu. Mwajua, watu walihurumiana nyakati hizo, tofauti na wanavyojisikia sasa. Mnajua, hakuna upendano mwingi miongoni mwa watu tena, hakuna ushirika.

75 Haijakuwa muda mrefu sana uliopita, nilikuwa katikati ya mji pamoja na mke wangu, na kulikuwa na mama mmoja aliyesema, "Halo, Dada Branham." Wala kamwe sikumsikia akisema neno.

Nikasema, "Mpenzi, mama huyo alikuzungumzia."

Akasema, "Nilimzungumzia."

Vema, nikasema, "Nina hakika yeye hakukusikia, sababu mimi sikukusikia, nami nimeketi karibu kuliko yeye alivyokuwa."

"Loo," akasema, "Ni—nilitabasamu kwake."

76 "Loo," nikasema, "upuuzi, Mpenzi. Maskini tabasamu la kijinga, halichukui mahali pa 'Halo hapo! U hali gani'?'" Hilo kamwe halitachukua mahali hapo. Hiyo ni kweli.

77 Watu wamefikia ambapo wanajaribu hata kuweka kitu kingine badala ya kupeana mikono vizuri.

78 Nilikuwa huko Florida miaka kadhaa iliyopita, nasi tulikuwa na mkutano mkubwa kwenye hema huko nje kwenye

Flagler Dog Track, ama huko nje kwenye Mtaa wa Flagler. Na kulikuwako na mvulana mdogo aliyekuwa huko chini, maskini mhubiri, alikuwa ni David, huko chini kwenye hema, naye alikuwa ameniomba nishuke nije nimsaidie. Alikuwa ameingia katika shida kidogo, nami nikashuka nikaenda nione kama ningeweza kumsaidia maskini jamaa huyo. Nao watu walikuwa wamesongamana sana mle ndani hata ilikuwa vigumu kwangu kuingia na kutoka bila watu watatu au wanne kusaidia kunisukuma ndani. Nao watu wagonjwa . . .

79 Hapo ndipo Ndugu Bosworth alipoingia katika huduma hii, akasema, "Hilo ndilo nimeombea tangu nilipokuwa mvulana."

80 Alipomwona Roho Mtakatifu akitokea mkutanoni, na kusema, "Wewe unayeketi hapo nje, wewe ni . . . " Mtu ambaye aliangushwa na farasi miaka michache kabla ya hapo, na mkono wake ukavunjika. Kasema, "Ulikuwa umepanda farasi Jumapili alasiri, ukienda mbio. Ulikuwa na soko la matunda hapa chini. Huyo farasi akakutupa, nawe hujawahi kusogeza mkono wako tangu wakati huo."

Naye akasema, "Hiyo ni kweli."

Kasema, "Nyosha mkono wako, Yesu Kristo anakuponya." Na hapo mkono wake ukanyoka.

81 Mzee Ndugu Bosworth akakimbia kule, na kusema, "Hilo ndilo nimetazamia! Loo," akasema, "Nimeyachunguza Maandiko kwa ajili ya jambo hilo." Bila shaka.

82 Ndipo kwenye mkutano huo, wakasema, "Ndugu Branham, mwanamke mwinyi anataka kukuona."

Nikasema, "Ati *nini*?"

Kasema, "Mwanamke mwinyi."

Nikasema, "Si—sijui unachozungumzia."

Naye akasema, "Vema, ni mwanamke mashuhuri, yeye ni mwanamke mwinyi." Kisha kasema, "Yuko moja kwa moja nyuma ya hema hapa."

Nikasema, "Vema, kwa nini nimwone? Vipi kuhusu wagonjwa hawa wote waliolala hapa nje?"

Naye . . . Wakasema, "Loo, lakini anamiliki kitu hiki chote kote hapa."

Nikasema, "Vema, Baba yangu anamiliki kitu hiki chote hapa. Mnaona?" Nikasema, "Kwa nini—kwa nini nimwone?"

Nikasema, "Wale ni watoto Wake wamelala huko nje wagonjwa, Naye alinituma hapa kuwaombea. Kama ninaweza kumwona mtu yeyote, acheni niwaone."

83 Kwa hiyo nilipotoka nje, walikuwa na mwanamke amesimama pale, kama ulisema hivyo au la. Mwanamke mkubwa mno, alikuwa na almasi za kutosha mkononi mwake kuwatuma wamishenari kote ulimwenguni mara hamsini,

hujawahi kuona dhahabu nyingi hivyo na kadhalika. Naye huyo mwanamke alikuwa na mi—miwani mkononi mwake, alikuwa na, alikuwa na miwani nchani mwake, ama, kijiti, akaiinua namna *hii*, akachungulia chini kupitia *hapa*. Sasa, unajua ya kwamba akili yoyote ya kawaida ingekwambia, hutaona kupitia miwani ikiwa mbali namna *hiyo*, ukiishikilia namna *hiyo*.

Ndipo akasema, "Je, wewe ni *Dk*. Branham?"

Nikasema, "La, mama, sivyo."

Akasema, "Vema, niliambiwa kwamba ulikuwa *Dk*. Branham, yule mponyaji wa Kiungu."

Nikasema, "La, mama, mimi ni Ndugu Branham, mtumishi wa Kristo."

84 Naye akasema, "Vema, *nimevutiwa*," ama nimefurahishwa, ama kitu kama hicho, huku ameinua mkono wake namna *hii*.

85 Nikamwangalia kidogo, nami nikawazia, "Hiyo ndiyo ya kuchekesha sana . . . Hatupeani mikono namna hiyo huko Kentucky."

86 Kwa hiyo, ni—niliona alitaka kupeana mikono nami, kwa hiyo nikanyosha mkono nikaushika mkono wake, nikasema, "Vema, ushushe hapa chini, nipate kukujua nitakapokuona tena." Mnaona? Mnaona?

87 Ni kitu gani? Ni mtu fulani anayejaribu kujifanya kitu wasicho. Hiyo ni kweli kabisa. Ni kujifanya sana ambako hakuna maana hata kidogo. Alikuwa si zaidi ya futi sita za mavumbi, kama sisi wengine, hiyo ni kweli hasa, bali akijaribu kujifanya kitu *fulani*, mnaona.

88 Kama vile maskini Mbunge Upshaw aliyeponywa mkutanoni, baada ya kuwa kwenye kiti cha magurudumu na mikongojo kwa miaka sitini na sita, daima alikuwa na msemo mdogo, alisema, "Huwezi kuwa kitu usicho." Na hiyo ni kweli hasa, jambo—jambo ndilo hilo, huwezi kuwa.

89 Loo, watu sasa, mwajua, hata hujui jirani ya—yako anapokufa, isipokuwa ulione kwenye gazeti. Hawana ushirika tena kama tuliokuwa nao. Tunaenda mbio barabarani maili tisini kwa saa, na kupiga kona, kisha tunasimama, na kuzungumza kwa saa moja kabla hujaenda nyumbani. Loo, kuna—kuna kitu fulani cha kichaa kuhusu kitu hicho chote. Lakini watu katika siku hizo walipendana, walikuwa na wakati, ushirika, na—na, kuzungumzana wao kwa wao.

90 Basi Elisabeti akamwona binamu yake, naye akatoka mbio, na kumkumbatia, akaanza kumkumbatia, akasema, "Loo, Mariamu! Mbona mara ya mwisho nilipokuona, ulikuwa msichana mdogo, mwenye mabakamabaka usoni, wewe huyu hapa, mwanamke mrembo. Na sasa, nilisikia kwamba ulikuwa unatembea na Yusufu, yule mvulana mzuri."

Akasema, “Naam, hiyo ni kweli, Elisabeti.”

91 “Vema,” akasema, “Nina furaha sana kukuona. Mbona, mpenzi, mbona usije uketi chini, mbona Yusufu ameenda kuchota maji, nipate kuitawadha miguu yako, lazima umechoka, inatokwa na damu. Kuna shida yoyote? Je, una haraka? Unaonekana kuwa na furaha sana, lakini hata hivyo unaonekana kana kwamba umekuwa na haraka.”

92 “Loo,” anasema, “Elisabeti, siwezi tu kungoja kukwambia! Loo,” akasema, “unajua, nitapata Mtoto.”

“Loo, kwani wewe na Yusufu tayari mmefunga ndoa?”

“La, bado hatujafunga ndoa.”

“Vema, Mariamu, nimeshtuka!”

93 “Loo, lakini Elisabeti, nikienda zangu kisimani, juzi asubuhi, nilikuwa ninatembea nikiwazia juu ya Maandiko ambayo mimi na Yusufu tulikuwa tukizungumzia siku iliyotangulia, nami nikaona Nguzo kubwa ya Moto imesimama mbele yangu, Gabrieli akaja kutoka ndani Yake, yule Malaika wa Mungu, ambaye aliniita kwa jina langu, na kuniambia ya kwamba nimepata neema mbele za Mungu, ya kwamba Roho Mtakatifu atanitia uvuli, na kwamba nguvu za Mungu zitakuwa juu yangu, nami nitapata Mtoto, Naye ataitwa Mwana wa Mungu.” Kisha kasema, “Yeye aliniambia kwamba wewe utapata mtoto pia, uzee hivi, na akasema tayari ulikuwa na miezi sita.”

94 “Loo,” akasema, “Mariamu, hiyo ni kweli. Mimi ni mja mzito, lakini, kipenzi, nina wasiwasi sana! Tayari nina mimba ya miezi sita, na huyu mtoto hajawahi kusogea, bado hajapata uhai hata kidogo. Nami nina wasiwasi sana juu yake.”

95 Loo, ninaweza kumsikia Mariamu akisema, “Usiwe na wasiwasi, kwa sababu kila kitu kitakuwa sawa, Malaika huyo alikujua na akalitaja jina lako, pia, ‘binamu yako, Elisabeti.’ Loo, kila kitu kitakuwa sawa. Naye akaniambia . . . hata alinipa Jina la Mtoto wangu.”

“Loo, alikupa?”

“Naam, alinipa Jina la Mtoto wangu, alisema ninapaswa kumwita Jina Lake *Yesu*.”

96 Yapata wakati tu aliposema, “Yesu,” kwa mara ya kwanza ambapo Jina hilo liliwahi kutajwa kwa midomo ya binadamu, mtoto Yohana alimpokea Roho Mtakatifu, na akaanza kuruka na kupaza sauti katika tumbo la mama yake. Loo, jamani! Maskini Yohana akaanza kurukaruka katika tumbo la mama kwa furaha.

97 Kama Jina la Yesu Kristo, mara ya kwanza lilipopata kunenwa kupitia midomo ya wanadamu, lilimfufua mtoto mchanga aliyekufa ambaye hakuwa amewahi kupata uhai, likamfufua, linapaswa kufanya nini na kanisa hili usiku wa leo,

pamoja na kundi la watu waliozaliwa mara ya pili waliojazwa na Roho Mtakatifu, huku Malaika wa Bwana akiwa hapa, kila usiku, akijionyesha Mwenyewe, ya kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele? Jina hilo tukufu la Bwana Yesu!

Loo, kuna nguvu, nguvu, nguvu zitendazo maajabu,
Katika Damu ya thamani ya Mwana-Kondoo.

98 Jinsi Jina hilo kuu, la ajabu, lisilo na dhambi, Jina hilo la Bwana Yesu lisiloelezeka!

99 Siku moja nililipa changamoto, nilitaka kuona kile nilichokuwa nikizungumzia. Nilipokuwa huko Ufaransa, nilienda Pigalle. Kamwe siamini neno la mtu yeyote kupahusu, nilitaka kujionea mwenyewe.

100 Waliniambia kuhusu umizimu, nami nikachukua jamaa kadhaa nikapanda kwenda Indiana, ambako walikuwa na ule mkutano mkubwa wa mizimu. Nilifikiri ilikuwa ni udanganyifu waliofanya. Basi nikaingia mle ndani, nao walikuwa na meza imesimama, na kusema, "Hakuna mtu anayeweza kuiangusha meza hiyo." Wakiendelea namna hiyo, nao watu walikuwa wakipiga makelele, na nguvu za pepo za kila namna.

101 Nao wakaangalia huku, nami nikasema, "Nguvu za Mungu zinaweza kuiangusha meza hiyo." Kisha nikasema . . .

102 Wasingeamini jambo hilo. Nao walikuwa wakijaribu kuishikilia kwa mikono, wanaume wanne huku miguu yao imefunikwa, wakijaribu kuivuta chini. Huku mwanamke huyu amesimama pale akifanya mambo ya kila namna, na kuifanya meza hiyo itembee, na ifanye kuzunguka. Nami . . . Walisimama niliposema jambo hili. Na mhudumu mwingine, Bw. DeArk, amesimama karibu nami.

103 Nikasema, "Kwa jina la mbingu juu, anguka."

104 Haikuanguka.

105 Nikasema, "Kwa jina la kanisa takatifu, anguka."

106 Haikuanguka. Niliita majina ya kila namna ambayo ningeweza kuwazia.

107 Baada ya kitambo kidogo nikasema, "Katika Jina la Yesu Kristo, anguka."

108 Na nusura ivunjike hiyo miguu ikigonga sakafuni! "Katika Jina Langu, watatoa pepo." Kuna nguvu katika Jina hilo.

109 Lilimfanya mtoto huyu mchanga kufufuka katika tumbo la uzazi la mama yake, na kuruka kwa furaha. Nayo Biblia ilisema ya kwamba Yohana alizaliwa kutoka tumboni mwa mama yake amejaa Roho Mtakatifu. Isitoshe, bali wakati alipokuwa katika tumbo la uzazi na Roho Mtakatifu juu yake, mama yake mwenyewe alimpokea Roho Mtakatifu, naye akatabiri akisema . . . akatoa unabii juu yake, na kuhusu Bwana Yesu.

110 Hivi hamwoni, enyi marafiki, Yesu Kristo yeye yule aliyezaliwa na bikira Mariamu, alizaliwa na bikira, Roho Wake Mtakatifu yuko hapa usiku wa leo? Yeye ana kila Malaika chini ya mamlaka Yake, ana kila nguvu chini ya mamlaka Yake. "Kila, mamlaka yote mbinguni na duniani," Yeye alisema, "yametiwa Mikononi Mwangu. Basi enendeni mkawafundishe mataifa yote, ulimwenguni mwote." Yeye—Yeye . . . Nguvu zote ziko ndani Yake, Naye aliahidi ahadi hizi. Usimhoji tu, liamini Neno Lake. Fanya hivyo tunapoinamisha vichwa vyetu, kwa muda kidogo tu sasa, kwa ajili ya maombi.

111 Ni wangapi wangetaka kukumbukwa, na kusema, "Ndugu Branham, jalia nguvu hizo zilizomfanya Yohana katika tumbo la uzazi la mama yake afufuke, jalia ziniamshe hisi zangu hafifu."

112 Mungu awabariki, enyi wavulana. Mungu awabariki hapo. Mungu awabariki, kote jengoni, mikono imeinuliwa. "Roho Mtakatifu na aniamshe kutoka kwenye usingizi huu ninaoketi. Ninataka kujazwa na Roho Mtakatifu kwa njia ambayo hisi zangu za kibinadamu hazitafanya kazi, isipokuwa iwe ni katika mapenzi ya Mungu. Ninataka kuongozwa na Roho."

113 Roho ni hisi ya sita. Mungu alimpa mwanadamu hisi tano, hazikuwa za kukutawala, ni za kuwasiliana na makazi yako ya duniani. Lakini hisi ya sita, ambayo ni imani, inakuongoza, inakutawala.

114 Baba yetu wa Mbinguni, loo, jinsi ilivyo vizuri kuzungumza juu ya Bwana Yesu, kuona jinsi inavyozibariki nafsi yetu, na kujua usiku wa leo ya kwamba kamwe hapajakuwa na mtu aliyezaliwa chini ya Mbingu namna hiyo! Kamwe hapajakuwapo na Zawadi ya ajabu kama hiyo iliyowahi kutolewa kwa ulimwengu wakati, "Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, kila amwaminiye asipotee, bali awe na Uzima wa Milele."

115 Yote ambayo Mungu ameifanyia jamii ya binadamu, nasi tuliketi na kurudia hayo tena katika matukio ya watu wengine wa zamani za kale, ambao wamekuwa na mawasiliano na Mbinguni kupitia wajumbe wa Malaika, na Bwana Yesu, na Roho Mtakatifu, na Mungu Mwenyewe.

116 Ee Bwana, tunaposhiriki mambo haya, na kujua ya kwamba si hadithi ya namna fulani, namna fulani tu ya hadithi ya kubuni, ama ushirikina miongoni mwa watu, bali Yeye yu hai usiku wa leo; Yeye yupo hapa usiku wa leo halisi tu kama alivyokuwa huko Galilaya. Hawezi kushindwa, Jina Lake limetolewa juu ya kila jina Mbinguni na duniani, jamaa yote inaitwa Yesu.

117 Mamlaka yote Mbinguni na duniani yamewekwa Mikononi Mwake, Naye alisema, "Enendeni mkaihubiri Injili. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

118 Usiku baada ya usiku Yeye ametuonyesha hapa, ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu yeye yule aliyeshuka na kujiumbia

Mwenyewe mwili, na kuzungumza na Ibrahimu, na kufanya ishara ya kujua ya kwamba alikuwa na mke, na jina lake lilikuwa Sara, na akajua ya kwamba alicheka hemani nyuma Yake. Mwili huo haukuwa kitu ila udongo, mavumbi, na nurulimwengu, na petroli, ulirudi moja kwa moja mavumbini mahali ulikotoka wakati alipomalizana nao; vivyo hivyo miili yetu itarudi moja kwa moja mavumbini tena. Hakuna kitu ndani yetu, Bwana, ila kwamba Roho Mtakatifu huyo mkuu angeweza kuangalia chini apate kujidhihirisha Mwenyewe, na kuthibitisha Neno Lake pamoja nasi, kuthibitisha ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

119 Tukiona hilo likitimia, basi, Bwana, tunawaleta wagonjwa usiku wa leo kwenye jukwaa hili kuwawekea mikono na kutamka baraka Zako. Kama tukiweka mikono juu ya kitu ambacho Wewe umelaani, Mungu zuilia baraka Zako. Lakini kama kila mtu ametubu dhambi zao, nao wako tayari kukupokea Wewe, ninaomba ya kwamba utamponya kila mtu aliye katika Uwepo wa Kiungu usiku wa leo. Tujalie, Bwana.

120 Hawa walioinua mikono yao muda mfupi tu uliopita, Bwana, naomba, wakati mkutano ukiendelea usiku wa leo, watapokea nguvu za Roho Mtakatifu, hata ataziua sana dhamiri zao za duniani hata watamtafakari Yeye, waimbe juu Yake, wazungumze juu Yake, mpaka Yeye atakapowatokea, Bwana, na kuwabadilisha. Tujalie.

121 Tunayakabidhi yote Kwako sasa, tukiutazamia Mkono Wako mkuu kutenda mambo haya ambayo Neno Lako limeahidi, nasi tumeomba. Katika Jina la Bwana Yesu, tunaomba. Amina.

122 Mnampenda? Loo, Yesu huyo wa ajabu, Mwana huyo wa Mungu aliyeshuka hivyo, na kujifanya Mwenyewe mwanadamu hata angeweza kushika mauti, akashika mwiba wa mauti katika mwili Wake na kuung'oa, uchungu wa mauti haungetudhuru kamwe! Tuko huru kutokana nao.

123 Hebu tuimbe wimbo wetu mzuri wa kale, *Nampenda*. Vema, mwanangu, hebu tuendelee. Sasa kila mtu aimbe tunapomwabudu, ujumbe umekwisha, mstari wa maombi uko karibu kuitishwa. Hebu tuimbe sasa:

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
. . . mtini Kalvari.

124 Na tuinamishe vichwa vyetu kwa utamu sana sasa, na kufunga macho yetu, na kuinua mikono yetu. Kama kweli tunataka kumwabudu Yeye, uimbeni kwa sauti ya chini sasa:

Nampenda, nampenda,
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

125 Sote pamoja sasa, pamoja na Sala ya Bwana:

> Baba yetu uliye Mbinguni, Jina Lako Litukuzwe.
> Ufalme Wako uje. Mapenzi Yako yafanyike duniani, kama huko Mbinguni.
> Utupe leo riziki yetu ya kila siku.
> Na utusamehe makosa yetu, kama sisi nasi tuwasameheavyo wanaotukosea.
> Na usitutie majaribuni, bali utuokoe na yule mwovu:
> Kwa kuwa Ufalme ni Wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.

126 Yesu alisema, "Unapoomba hiyo, kama una jambo moyoni mwako, msamehe kila mtu, kutoka moyoni mwako, kosa lake. Kwa maana usiposamehe, kutoka moyoni mwako, kila kosa alilofanya mtu dhidi yako, wala Baba yako wa Mbinguni hatakusamehe yako."

127 Kwa hiyo, ingia kwenye mstari huu, uwe huru na dhambi. Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, ombeaneni, mpate kuponywa.

128 Nitamwomba ndugu yetu sasa, wakati nikiitisha mstari wa maombi . . . Sasa, ninataka kuwaita tu mmoja mmoja, ili kwamba msije mkasababisha hali ya vurugu. Basi ni wangapi hapa walio na kadi ya maombi, sasa inueni mikono yenu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

129 . . . vuka tu bahari. Ndipo akatua katika nchi nyingine, ndipo maskini mwanamke mmoja akaja bila sifa yoyote, mtu yeyote kumleta. Miaka mingi alikuwa na mafuriko na kutokwa na damu, hakuna madaktari wangeweza kumtibu. Labda alikuwa ameuza yote aliyokuwa nayo kuwalipa waganga, nao walikuwa wamejaribu sana, lakini walikuwa wameshindwa. Lakini aliamini kama angeweza kugusa vazi Lake, angepona. Basi akapitia kwenye umati wa watu, akaligusa vazi Lake.

130 Sasa, vazi la Kipalestina lina vazi la ndani na joho linalopwaya. Naye akagusa upindo, ambao labda ungekuwa mbali *hivyo* kutoka Kwake, umening'inia. Naye akaugusa upindo kwa kidole chake, akarudi kupitia kwenye umati na kuketi chini, akasimama, ama chochote alichofanya.

Yesu akasimama, na kusema, "Ni nani aliyenigusa?"

131 Wazia tu jambo hilo sasa. Sasa kumbukeni, tunazungumza juu ya Yesu. Kila kitu katika mstari wa uponyaji, nionavyo mimi, hakina budi kuwa ni cha Kimaandiko, hakina budi kuwa juu ya Biblia, hakina budi kuwa kile alichokuwa Yeye, kile alichofanya, kile tu alichofanya, basi Yeye Ndiye tunayemtazamia leo. Yeye Ndiye aliyeahidi kuwa hapa, yeye yule jana, leo, na hata milele.

132 Kuna wageni wowote hapa ndani ambao hawajawahi kuwa katika mmoja wa mikutano hapo kabla? La, nadhani... Mwanamke mmoja, wawili, watu wawili ninaowaona. Vema.

133 Kwa hiyo, yule mwanamke akamgusa, akarudi na kuketi chini, naye ameketi pale, Yesu akasema, "Ni nani aliyenigusa?

134 Ndipo Petro akaja, na kumkemea tu waziwazi Biblia ilisema. Mbona, ningewazia huyo mtume alisema kitu kama hiki: "Unamaanisha nini kwa kusema jambo kama hilo? Mbona, hawa hapa watu mia tano, na kila mmoja wao anakugusa Wewe!"

135 Yesu akasema, "Lakini nimekuwa dhaifu, nguvu zimenitoka." Ndipo akaangalia kote katika kusanyiko, akamwona yule mwanamke, na kumwambia kutokwa kwake na damu kulikuwa kumekoma, kwa sababu imani yake ilikuwa imemponya. Hiyo ni kweli?

136 Sasa, ni wangapi wenu ninyi wahudumu na wasomaji wa Biblia mnaojua ya kwamba Biblia, Agano Jipya, lilisema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele"? Ni wangapi wanaojua ya kwamba Yeye, Biblia ilisema ya kwamba sasa hivi yuko kwenye mkono wa kuume wa Mungu katika ukuu huko Juu, mwili Wake halisi umewekwa pale, Kuhani Mkuu, akituombea tunapokiri, Naye anaweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu? Biblia ilisema hivyo.

137 Sasa, mwili Wake uko juu kule, Roho Wake yuko hapa chini. Roho Wake—Wake, Roho wa Mungu, alitenda kazi kupitia mwili huo, Mwanawe aliyezaliwa na bikira, katika utimilifu wa Mungu; Yeye hufanya kazi kupitia mimi na wewe kama sehemu za Mungu. Hiyo ndiyo sababu Roho Mtakatifu, alipokuja kwenye Siku ya Pentekoste, alivunjika-vunjika kabisa, ile Nguzo ya Moto, na kujigawa Mwenyewe katika Miale ya Ndimi, na kukaa juu ya kila mmoja. Hatuna budi kushirikiana sisi kwa sisi.

138 Jambo kubwa sana ibilisi alilopata kutushindia ni wakati alipotutenganisha na upendo wa Mungu, mmoja na mwingine. Nasi tunapendana, huo ni upendano wa ndugu. Tunapoweza kupatana... Kama una sehemu ya Roho Mtakatifu, nami nina sehemu Yake, mtu mwingine ana sehemu Yake, tukiwekwa pamoja, hizo hapo sehemu tatu. Nina nguvu mara tatu kuliko nilivyokuwa nikiwa nanyi ndugu wawili. Mnaona? Hivyo ndivyo tunavyosimama. Mimi ni Mkentaki halisi, "Pamoja tunasimama, tukigawanyika tunaanguka." Hiyo ni kweli. Hatuna budi kusimama hivyo pamoja.

139 Sasa, kama Yesu Kristo ni Kuhani Mkuu yeye yule ambaye mwanamke huyo alimgusa kwa mambo ya udhaifu wake, Naye ni Kuhani Mkuu yule yule, atatenda vile vile, atafanya vile vile kama unaweza kumgusa. Sasa leo, Yeye ananinii tu... Huwezi kumgusa kwa kidole chako, huna budi kumgusa kwa imani yako. Hiyo ni kweli, ndugu? Hiyo ni kweli? Imani yako

ndiyo inayomgusa Yeye. Huwezi kumgusa kwa kidole chako, kwa sababu Yeye ameketi kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu.

140 Ni wangapi wanaoamini ya kwamba Yesu alishinda na kuketi kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, na akaahidi ya kwamba kama tukishinda, tutaketi pamoja Naye kwenye kiti Chake cha enzi, kama Yeye alivyoshinda na kuketi kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu? Ndivyo hasa alivyosema. Vema.

141 Basi kama hiyo ni kweli, basi kama ninyi, usiku wa leo, mko huko nje, hizi hapa kadi zote za maombi, wanaosimama, nawe uko huko nje bila kadi za maombi, nawe utaamini kwa moyo wako wote ya kwamba imani yako inaweza kumgusa, nawe unaamini, basi Mungu atajibu na kutenda kama tu vile Kuhani Mkuu alivyofanya hapo mwanzo. Unaamini hilo?

142 Je, umefanyiza, mstari wote wa maombi? Kadi zote hamsini za maombi basi. Hiyo B moja hadi hamsini, ulisema? Sawa.

143 Sasa usiku wa leo, sababu ya mimi kuliita kundi lote, huu si mstari wa upambanuzi, huu ni mstari wa kuwaombea wagonjwa. Mnaona? Upambanuzi huja kila usiku mikutanoni. Lakini Yeye yupo hapa vilevile. Mnaamini hilo? Hakika, Yupo. Kama hamna jambo moja lililofanywa, Yeye angali hapa kuwaponya wagonjwa kama mtaamini. (Asante, Paul.)

144 Ni wangapi huko nje ambao bado ni wagonjwa, hebu tuone mikono yenu. Kama . . . Ni wangapi huko nje mlioinua mikono yenu mnaoamini ya kwamba wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, kwamba jinsi alivyojitambulisha Mwenyewe kuwa Masihi, angeweza kuwaambia watu shida yao ilikuwa ni nini, na kadhalika? Ni wangapi wanajua hilo, wanajua ya kwamba hiyo ni ahadi ya Biblia? Vema basi, mnajua ya kwamba nisingeweza kuwa Yeye, kwa sababu Yeye ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Lakini Yeye aliahidi kazi alizofanya, sisi nasi tungezifanya pia.

145 Yeye aliahidi katika siku za mwisho ya kwamba Kanisa lingefanana sana, tangu siku za Luther, kuhesabiwa haki; siku za Wesley, utakaso; siku za Pentekoste, kule kurudishwa kwa karama; moja kwa moja hadi kwenye lile Jiwe la Kifuniko, na kupitia hilo lingeuleta Mwili wote, ule ufufuo wa kila mwaminio.

146 Lakini kadiri Ro—Roho wa Mungu anavyozidi kukaribia, kama tu kivuli cha mkono wangu, kivuli huzidi kuwa cheusi, cheusi zaidi, cheusi zaidi, mpaka hicho ki—kivuli na mkono vinakuwa kitu kile kile. Kanisa limetoka kwenye kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, sasa linaingia kwenye lile Jiwe lenyewe la Kifuniko na Mbele za Malaika wa Mungu, Yesu Kristo, Roho Mtakatifu yupo sana, akifanya kazi zile zile alizofanya duniani, ambalo linalileta Kanisa na Kristo kuungana pamoja. Yale hasa aliyoahidi. Sasa, usiache dhamiri yako iwe nzito sasa, amka.

147 Sasa, Baba wa Mbinguni, niliwaahidi hawa watu kuwapitisha tu kwenye mstari huu wa maombi na kuwaombea. Lakini ninakuomba Wewe, Baba, ya kwamba utamjalia angalau mtu mmoja ama wawili mahali fulani hapa ndani kwamba watashuhudia, kwa sababu kuna wengine hapa ambao hawajapata kujua ya kwamba jambo hili, ni mikono miwili tu iliyoinuliwa ambao hawakuwa wamewahi kuwa mikutanoni hapo kabla, lakini Bwana, hao huenda wakawa ndio hao watu wawili unaowaita usiku wa leo.

148 Kwa hiyo, kuwa na hakika, kwamba kwenye Siku ya Hukumu sitaki chochote ambacho nimeacha bila kutekeleza, ninakuomba, Baba, kwa dakika chache, ya kwamba kama utamtuma Roho Mtakatifu Wako miongoni mwa watu hao, na kuichochea miili yao walipoinua mikono yao muda mfupi uliopita, ya kwamba utafanya kazi zile zile hapa ulizofanya, kama yule mwanamke kisimani ulipozungumza naye, mwanamume na mwanamke, na ukamwambia mahali siri yake ilipokuwa, kilichokuwa shida yake.

149 Mbona, akasema, "Bwana, naona kwamba Wewe ni Nabii. Tunajua ya kwamba Masihi ajapo, Yeye atatwambia mambo haya."

150 Naye akasema, "Mimi ninayesema nawe Ndiye."

151 Akakimbia mjini na kuwaambia hao watu, "Njoni, mwone Mtu ambaye ameniambia mambo niliyofanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?"

152 Mungu, tujalie tena, usiku wa leo. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

153 Kila usiku nimekuwa nikilipa kusanyiko kisogo, mpate kujua, na Mungu athibitishe ya kwamba ninii . . . Ni wangapi wanaojua ya kwamba Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu"? Yeye alisema hivyo.

154 Sasa, ni jambo gani lililotukia huko Sodoma? Sasa, Yeye alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, watu wanane waliokolewa kwa maji." Vema, mnaona mahali ambapo walio wachache watakuwa kabla kile Kifuniko hakijawekwa, lile Jiwe, likirudi. Sasa, Jiwe lile Kuu la Pembeni linaingia kwenye hilo Jengo na kulishikamanisha pamoja. Sasa, Yeye alisema jinsi hilo lingekuwa, alisema yale waliyokuwa wakifanya katika siku za Nuhu: kula, kunywa, kuoa, na kuolewa. Mnaona? Lakini alipofikia Sodoma, aliacha hilo ili Kanisa lipate kupambanua.

155 Sasa mnaona, kulikuwako na mwaminio, mshiriki vuguvugu wa kanisa, na asiyeamini. Naye Ibrahimu alikuwa ametoka Sodoma, ambalo linamaanisha Wateule na walioitwa watoke, Kanisa. Na yule mmoja . . . Malaika wawili walishuka kwenda Sodoma, wakafanya mambo machache, kama vile kupofusha, kuweka laana juu ya watu. Kwa mfuasi wa kanisa: walifanya

mkutano, wakaomba rehema ili watoke mbio, bali hawakufanya hivyo. Kama tu vile Ujumbe unavyoenezwa siku hizi.

156 Lakini kulikuwa na Malaika mmoja aliyekaa na Kanisa teule. Naye akamwambia Ibrahimu, sasa Yeye alikuwa ni Mgeni, akasema, "Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?" "Sara mkeo?" Mgeni. Mnaona?

Kasema, "Hemani nyuma Yako."

157 Kasema, "Sitakuficha hili." *Mimi*, kiwakilishi nafsi sasa, "Sitakuficha hili, bali katika muhula wake, Sara atakuwa kijana mwanamke tena," mmenisikia nikihubiri juu yake, "naye atarudi, amzae mtoto huyu."

158 Naye Sara hemani nyuma ya huyo Mtu, kamwe hakumwona Huyo, hemani akacheka moyoni mwake.

159 Naye huyo Malaika, huku amegeuza mgongo Wake, akasema, "Kwa nini Sara akacheka?"

160 Ibrahimu alimwita Elohimu, si yule mtu aliyeketi pale akila mnofu na kunywa maziwa, akila ugali wa mahindi, bali ilikuwa ni Roho aliyekuwa ndani yake. Sasa, ilikuwa ni ishara ya nini? Kwamba Roho wa Mungu atakaa katika miili ya watu tena na kuonyesha ishara ile ile kabla ya wakati wa mwisho. "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu."

161 Sasa, Sodoma ndio ulioteketea, Moto ulishuka kutoka Mbinguni na kuwateketeza. Na hilo ndilo litakalotukia tena, haitakuwa ni maji, itakuwa ni Moto. Kwa hiyo huyo Malaika wa rehema anakuja na Ujumbe ule ule kuwaonya watu, "Kaeni mbali na Sodoma!"

162 Sasa, wewe omba uone kama unaweza kugusa vazi Lake. Na hebu na aongeze baraka Zake.

163 Hebu kidogo, Billy. Ninawataka watu hawa hapa nje kwenye kusanyiko kwanza. Ndipo ninapoanzisha mstari huo . . . Kuwafanya tu wajue ya kwamba Roho Mtakatifu yupo hapa. Hao watu wana kadi za maombi. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

164 . . . wakisikiliza . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kuyachunguza Maandiko. Huwezi kukana ila kwamba haya ni Maandiko.

165 "Nami ninahitaji usiku wa leo, hebu na azungumze nami. Yeye hanijui, hebu aniambie ninaumwa nini, ama jambo fulani kunihusu mimi. Nitaamini, Bwana. Nitamwambia kila mtu aliyeko ambaye ninaweza kuwasiliana naye, ya kwamba Yesu Kristo yuaja hivi karibuni, Mwana wa Mungu, na Yeye ndiye Mponyaji mkuu."

166 Hii hapa. Yupo mwanamke aliyeketi papa hapa, akiangalia chini, akiomba. Aliinua kichwa chake kuniangalia, anaumwa na kichwa. Unaamini Bwana Yesu atakuponya, mama? Unayeketi

hapo, mwanamke wa pili kutoka mstarini, nyuma ya mstari hapo, unaamini ya kwamba Yeye atakufanya mzima? Unaamini hayo maumivu ya kichwa yatakoma? Kama unaamini, inua mkono wako. Vema, yatakuacha sasa.

167 Unaamini kwa moyo wako wote?

168 Hapa, mtu huyu aliyeketi papa hapa ameinamisha kichwa chake, akiomba, akiteseka kwa mkandamizo. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya na kukuondolea mkandamizo huo? Kama unaamini, inua mkono wako. Vema. Ulikuwa na imani zaidi ya ulivyodhania ulikuwa nayo, sivyo? Sasa, ibilisi amekuwa akikudanganya, sasa, unajua hilo, bali amekuacha sasa. Endelea, furahi tu, na uimbe, na kushangilia.

169 Mwaminini Mungu. "Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana." Mnaamini hilo? Biblia ilisema hivyo.

170 Mtu huyu hapa, aliyeketi hapa akiamini, pia. Lakini si yeye, kuna mtu mwingine anayeamini, siye mtu huyo. Ni mwanamke mweusi, anaugua ugonjwa wa moyo, ana mkandamizo, pia. Mungu nijalie kujua ni nani. Jina lake ni Bibi Hagwood. Uko wapi, Bibi Hagwood? Imani yako imekuponya, nenda nyumbani na uwe mzima, Yesu Kristo anakuponya.

171 Je, anabaki Yeye yule jana, leo, na hata milele? Sasa, siwajui watu hao, sijawahi kuwaona maishani mwangu, ni watu tu walioketi hapo. Sasa ninyi aminini, ninyi nyote, kwa moyo wenu wote, mwaminini Mungu.

172 Hatufahamiani, bwana. Sisi ni wanaume wawili waliokutana. Kama tu wakati mmoja, kulikuwa na mtu jina lake Simoni aliyemjia Bwana wetu. Na sasa, kwa kuwa wewe u wa kwanza hapa katika mstari huu: Kama Yesu Kristo ataniambia shida yako ni nini, utaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Utaamini. Unajua hatufahamiani, sivyo? Ili watu wajue, hebu na tuinue mikono yetu, ili kwamba wajue kwamba hatufahamiani.

173 Sijawahi kumwona mtu huyo, sijui lolote kumhusu. Sasa, yeye—yeye—yeye—yeye alikuwa na kadi ya maombi, nadhani, yeye yuko mstarini, alikuwa na kadi ya maombi, hao wengine hawana kadi za maombi. Mnaona? Ili muweze kujua kadi ya maombi haina uhusiano wowote nalo.

174 Sasa iweni na kicho sana sasa mkiweza, watulivu sana. Msisogeesogee. Mnaona, kila mmoja wenu ni roho, mnajua hilo.

175 Vema, sasa unaweza kuweka mkono wako chini na kutazama hapa. Kama Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele, basi atafanya vivyo hivyo. Ingekusaidia kama ningeweza, kwa Roho Mtakatifu, kukwambia shida yako ni nini? Hilo lingekusaidia? Bila kukujua, ingenibidi kuwa na njia ya kujua jambo hilo. Unaamini ingekuwa ni Kristo, kwa karama tu? Isingekuponya, bali ingekusaidia kuamini upate kuponywa, kwa sababu uponyaji wako tayari umefanywa. Haidhuru ningesema

nini, bado haingekuponya, bali ingeinua imani yako, kwa sababu unajua ya kwamba hatufahamiani.

176 Ingewasaidia ninyi wengine wote huko nje kuamini?

177 Huyo mtu anaugua ugonjwa wa damu, kisukari. Sawa. Sasa, unaamini? Ingekusaidia kama Mungu angeniambia wewe ni nani? Unajua sijui wewe ni nani. Ingekusaidia? Forrest Clair. Ingesaidia kukwambia unakotoka? Gilbert, Arizona. Rudi nyumbani sasa ukaponywe. Hiyo inakusaidia? Mungu akubariki, nenda ukiamini.

178 Una . . .? Unamwamini Mungu? Sasa na tuombe. Sasa kumbukeni, ninyi watu wote mlio kwenye mstari wa maombi huko nje, ombeni sasa. Sasa, msi—msitoke vitini mwenu, tafadhalini, ketini, nyamazeni tu kabisa, ombeni. Hujui yale Mungu anaweza kufanya hapa usiku wa leo. Sasa, upako wa Roho Mtakatifu ni mkubwa sana hapa sasa hivi, kwa hiyo mninii tu . . . Ninatazamia kitu fulani, kweli, kutukia sasa. Na sasa, angalieni hapa, ninyi watu wote mlio kwenye mstari wa maombi, kanisa hili lote limeahidi, wataamini na kuwaombeeni.

179 Sasa, njoni tu sasa ninapoomba.

Sasa, njoo dada.

180 Baba yetu wa Mbinguni, pamoja na kanisa hili ninaomba maombi ya imani juu ya dada yangu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Sasa, nenda ukiamini, ukiwa na imani.

181 Vema, njoo. Vema, unaamini sasa kwa moyo wako wote? Unaamini ya kwamba Mungu atauponya huo moyo, na mtoto mchanga, pia? Vema, basi unaweza kwenda, ukaponywe. Amini kwa yote yaliyo ndani yako sasa.

182 Vema, mlete. U hali gani, dada? Unaamini Yesu Kristo atakuponya?

183 Baba yetu wa Mbinguni, ninamwombea dada yetu, pamoja na kanisa hili, kwamba Wewe utamponya na kumpa afya. Kupitia Jina la Yesu. Amina.

184 Maandiko yanasema nini? "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." [Dada huyo anasema, "Nilisoma hayo nyumbani."—Mh.] Loo, u—unajua inahusu nini. Unaamini Yeye alikuponya sasa? Moyo hautakusumbua tena, na kitu hicho kitaondoka usoni mwako, na shida hizo zote zitakuwa—zitakuwa sawa sasa? Nenda zako ukishangilia, ukisema, "Asante, Bwana Yesu," na upate afya.

185 Sasa, wewe ni kijana mwanamke mzuri sana kuwa na wasiwasi jinsi ulivyo nao, bali hivi unaamini ya kwamba uliponywa papo hapo? Unajua. Vema, nenda zako tu, useme, "Asante, Bwana Yesu." Na uamini kwa moyo wako wote.

Unaamini kwa moyo wako wote, dada?

186 Baba yetu wa Mbinguni, ninamwekea mikono. Mikono yangu inawakilisha kanisa hili lote, jalia aponywe. Katika Jina la Yesu. Amina.

Amini, sasa.

187 Nisiposema neno moja kwako, hata hivyo unaamini utaponywa. Mnaona, upambanuzi huo ungeniua katika dakika chache tu, siwezi kuwapitia wote, mwajua.

188 Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya huyu mwanamke, na kuufanya moyo wake kuwa mzima. Katika Jina la Yesu. Amina.

Bwana akubariki.

Unaamini, dada, Yeye atakuponya?

189 Baba yetu wa Mbinguni, ninamwombea dada yetu, ya kwamba utamponya na kumpa afya. Katika Jina la Yesu. Amina.

Sasa nenda ukishangilia ukisema, "Asante, Bwana."

Nawe unajua huna budi kuamini, dada, la sivyo ufe.

190 Katika Jina la Yesu, ninamhukumu ibilisi huyu anayemwua dada yangu, na amwache. Katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu akubariki, dada.

Njoo, ndugu.

191 Baba Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba ya kwamba utamponya ndugu yetu na kumpa afya. Amina.

192 Sasa, amini, usiwe na shaka, amini kwa moyo wako wote.

193 Sasa, unajua ya kwamba ninajua shida yako, sivyo? U—unajua hilo, lakini kama hata nisiposema chochote, ninataka kuwatia moyo. Unaona? (Lakini yabisi kavu yako itakuwa sawa.)

194 Ee Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utambariki, na kumponya, na kumpa afya, kupitia Jina la Yesu. Amina.

195 Nenda, ukiamini sasa, kamwe hutalemaa.

196 Bwana wetu wa thamani, Biblia ilisema, ambayo Mwandishi Wake yupo, ilisema ya kwamba, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: Wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya." Watu hawa ni waaminio, mimi ni mwaminio, kanisa hili linaamini. Tunawawekea mikono katika Jina la Yesu, kwa ajili ya uponyaji wao. Amina.

Nenda, ukiamini sasa.

197 "Kama unaweza kuamini!" Je, wewe. . .? Mnaona, ninasema jambo hili moja kwa moyo wangu wote: Laiti nisingaliyatambulisha maono hayo kwa watu, niyaweke tu moyoni mwangu mwenyewe. Mnaona? Kama ukiwahi kuliona wakati mmoja, kila mtu anafikiri kwamba inawabidi kufanya hivyo, la sivyo hawajaponywa. Mnaona? Inalifanya kuwa baya.

Yeye angali yuko hapa, anajua yote kuwahusu. Hivi humwamini hilo? Bila shaka, Yeye anajua. Ninii tu . . .

198 Unaamini hilo, dada? Hakika, unaamini. Vema, kwa kuwa unaamini, nitakwambia ya kwamba kama utamwamini Mungu kwa moyo wako wote . . . Unajua uko—uko katika vivuli vya mauti. Hiyo ni kweli. ["Nina shida gani?"] Kansa kwenye ini. Una kansa kwenye ini. Hiyo ni kweli kabisa. Bibi Randall, nenda nyumbani na uamini kwa moyo wako wote, nawe utakuwa mzima. Unaamini hilo kwa moyo wako wote? Vema, nenda nyumbani na useme, "Asante, Bwana Yesu kwa kuniponya."

Njoo.

199 Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utambariki mtu huyu, na kumponya na kumpa afya, kwa ajili ya utukufu Wako. Katika Jina la Yesu. Amina.

Ubarikiwe, bwana.

200 Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utambariki dada yetu, na kumpa afya. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

201 Baba Mungu, ninaomba ya kwamba utambariki dada yetu, na kumponya. Katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Amina.

202 Sasa angalia, dada, utakuwa mzima. Unapoondoka hapa . . .

203 Wakati ninyi—wakati ninyi watu mnapokuja hapa, mnapoombewa, mmetimiza masharti. Mlikuwa hapa jana usiku niliposema, "Masharti yanapotimizwa, shikilia"? Mungu yupo kujibu, endelea tu kuamini.

Njoo, dada.

Baba Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba ya kwamba utamponya. Amina.

"Ishara hizi zitafuatana na hao . . . "

204 Loo, dada, ungetaka . . . Unataka kukwepa upasuaji huo? Unataka? Unaamini ya kwamba Mungu atakuondolea uvimbe huo? Nenda, na uamini kwa moyo wako wote.

Ee Baba Mungu, ninaomba ya kwamba utamponya na kumfanya mzima. Kupitia Jina la Yesu Kristo. Amina.

Amini, amini kwa moyo wako wote.

205 Sasa, umekohoa na ukaendelea na ugonjwa huo wa pumu karibu miaka na miaka. Unaamini Yeye atakuponya sasa? Je, hilo lilikusaidia? Vema, jambo ndilo hilo. Nenda na uamini kupitia Yesu Kristo.

Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamsaidia, na kumpa afya. Katika Jina la Yesu, lijalie, Baba.

[Dada mmoja anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Hakika atafanya hivyo. Mungu na ajalie haja yake, katika Jina la Yesu.

Mungu ambariki dada yetu aliyesimama hapa, ninaomba ya kwamba utamponya. Katika Jina la Yesu.

Mungu ambariki huyu anayemleta. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

206 Bwana ambariki huyu, ndugu yangu, na wakati kanisa hili linapomwombea, nguvu za Mungu na ziwe juu yake na kumponya. Katika Jina la Yesu.

207 Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu na kumpa afya, katika Jina la Yesu.

208 Je, umekubali uponyaji? Unaamini ya kwamba hutakuwa nao tena, nawe utakuwa sawa? Unaamini? Basi unaweza kurudi nyumbani kwako, na kuamini ya kwamba utapona. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina. Nenda, ukiamini.

Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utambariki mtu huyu na kumponya. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Njoo, dada mpendwa.

209 Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya na kumpa afya. Katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba. Amina.

210 Sasa amini. Hebu—hebu inua tu mkono wako, dada, useme, "Asante, Bwana Mungu."

211 Nyote mnaomba? Kila mtu anaamini kwa moyo wako wote?

212 Vipi kukuhusu wewe kwenye kiti cha magurudumu, unaamini? Vipi kuhusu wewe hapa, unaamini? Unaamini, sivyo, bwana? Unajua, tulizungumzia habari zake huko nyuma, shida yako.

213 Hapa, huyu hapa mwanaume. Njoo hapa. Mnamwona mtu huyu? Simjui, hatufanamiani. Hiyo ni kweli, bwana? Hatufahamiani. Hiyo ni kweli? Hebu tuinue mikono yetu, kusudi watu waone ya kwamba hatufahamiani. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani, kile ulicho, yale umefanya, ama shida uliyo nayo? Unaamini hilo? Je, lingekusaidia?

214 Ingekusaidia, bwana, kuamini ya kwamba unaweza kurudi na kupona, kutoka hospitalini? Unajisikia vizuri zaidi. Sasa, hiki ndicho kilichokufanya ujisikie vizuri zaidi: Mungu yeye yule Mbinguni anayeweza kunitumia kumwambia mtu huyu mambo ambayo Biblia iliahidi yatasemwa. Sisi hapa, sote wawili huku mikono yetu ikiwa mbele za kila mmoja, mbele za Mungu hatujawahi kukutana maishani tunayojua, mahali popote. Sasa niangalieni kwa dakika moja tu.

215 Vema, una namna fulani ya kuwashwa kila mahali, kunakusumbua. Umefanyiwa upasuaji, hiyo ilikuwa ni kansa, ilikuwa usoni mwako, ikarudi tena. Mkeo yuko pamoja nawe. Unaamini Mungu anaweza kuniambia mke wako ana shida gani, aliyeketi huko nje? Ungeamini? Kufunga choo. Hiyo ni kweli kabisa. Unaamini Mungu anajua wewe ni nani? Kama

ataniambia wewe ni nani, utamwamini? David Wood. Nenda nyumbani, ukaponywe, katika Jina la Yesu Kristo. Je, hilo lilikusaidia . . .?. . .

Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamsaidia na kumponya. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamsaidia na kumponya, katika Jina la Yesu.

Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya, katika Jina la Yesu Kristo.

Mungu, wabariki, na uwaponye, katika Jina la Yesu Kristo.

Usijali, usijali. Itakuwa, najua, itakuwa sawa, amini tu.

Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utambariki kijana huyu, na kumponya na kumpa afya. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Njoo, dada yangu.

Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya na kumpa afya. Kupitia Jina la Yesu. Amina.

Njoo, ndugu yangu.

Katika Jina la Yesu Kristo, Roho Mtakatifu mkuu na amponye. Amina.

Njoo, ndugu yangu.

Katika Jina la Yesu Kristo, Roho Mtakatifu wa Mungu na amponye na kumfanya mzima.

Unaamini uliupokea?

Unamwamini Yeye? "Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana." Hiyo ni kweli?

216 Unaamini, ewe jamaa mdogo? Tumbo hilo halitakusumbua tena sasa, unaweza kwenda nyumbani, unaona, itakuwa sawa.

217 Vema, dada. Hatufahamiani. Hutoki Phoenix. La, umetoka mbali na hapa. Umetoka jimbo jingine, na jimbo lako upande wako wa magharibi linakabili eneo kubwa la maji, ni Ziwa Michigan. Basi nenda na uamini sasa kwa moyo wako wote, na huko kunguruma kichwani mwako, ugonjwa huo wa tumbo, na kadhalika, unaamini ya kwamba Mungu atauponya? Unaamini itakuwa sawa? Una mpendwa unayemwombea, ni binti, yuko katika hospitali ya wendawazimu. Hiyo ni kweli. Sasa unaona, hakuna siri mbele za Mungu. Nenda, ukiamini na upate afya.

Baba yetu wa Mbinguni, ninamwombea mwanamke huyu kwamba utamponya, katika Jina la Yesu.

Njoo, ndugu yangu.

Katika Jina la Yesu Kristo, ndugu yangu na aponywe kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

Njoo, dada mpendwa.

Katika Jina la Yesu Kristo, dada yangu na aponywe. Amina.

Angalia watu wanaokuombea, dada.

Katika Jina la Yesu Kristo, naomba uponywe.

Njoo, dada.

Katika Jina la Yesu Kristo, naomba uponywe.

Njoo, ndugu yangu.

Katika Jina la Yesu Kristo, naomba uponywe.

Biblia ilisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya ndugu yetu. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Njoo, dada mpendwa.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia huyu, dada yangu, aponywe kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Amina.

Njoo, dada, mwamini kwa moyo wako wote.

218 Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utunzaji Wako wenye rehema utakuwa pamoja na mwanamke huyu ninapomwekea mikono. Jalia ibilisi ambaye amemfunga wakati huu wote, amwache, katika Jina la Yesu Kristo.

Nenda ukiamini.

219 Ee rehema, mwanamume kipofu. Inamisheni vichwa vyenu kwa muda kidogo tu.

220 Unaamini Bwana Yesu atakusaidia, na kuyafungua macho yako? Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini? Upofu, udhaifu, na kadhalika, hiyo ni kweli? Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu, na kumwomba Yeye awasaidie.

221 Baba yetu wa Mbinguni, katika Jina la Bwana Yesu, mrudishie mtu huyu uwezo wake wa kuona. Udhaifu na uondoke mwilini mwake, na awe na nguvu, macho yake na yamrudie. Hatuombi miujiza, Bwana, Ulisema, "Ki—kizazi dhaifu na cha zinaa hutafuta mambo kama hayo." Lakini, Bwana, tunajua ya kwamba Wewe hufanya miujiza. Nami ninaomba ya kwamba utayafungua macho yake, kupitia Jina la Yesu. Amina.

222 Sasa, angalia huku. Kama . . . Unaweza kuniona sasa? Vizuri kuliko ulivyoniona? Anaweza kuona, macho yake yamefunguliwa. Weka mikono yako juu ya pua yangu, na kuwaonyesha watu ya kwamba unaweza kuona. Vema, unajisikia mwenye nguvu zaidi? Vema, ondoka jukwaani, utakuwa mzima, utaponywa.

223 Unaamini kwa moyo wako wote? Vipi kuhusu wengine wenu huko nje, mnaamini?

224 Wewe uliyeketi kwenye hicho kiti cha magurudumu, unamwamini Mungu? Umekuwa ukiniangalia hapa kwa muda

mrefu, umekuwa ukiwazia moyoni mwako, “Mtu huyo yuko sahihi.” Je, hivyo ndivyo umekuwa ukiwazia? Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Ni kweli. Unaamini sasa hivi kwamba ninajua shida yako. Unaamini? Nikikwambia, je, utasimama, na kwenda nyumbani, uisahau? Hiyo mizio na kadhalika itakuacha basi. Simama, uende nyumbani. Unaamini kwa moyo wako wote? Simama na umwamini Mungu, chukua mkokoteni wako, na uende nao nyumbani, katika Jina la Yesu Kristo.

225 Mnaamini, ninyi wengine? Huyo hapo anaenda, kutoka kwenye kiti cha magurudumu.

226 Mungu awabariki, kila mahali, nenda nyumbani na uwe mzima.

227 Ni wengine wenu wangapi wanaotaka kuamini? Simameni kwa miguu yenu, simameni na mliamini. Sijali, ninyi mlioketi hapo, hata uwe nani, katika Jina la Bwana Yesu Kristo, inueni mikono yenu na mumpe Mungu sifa. Mungu awabariki, kila mmoja. Roho Mtakatifu anawaponya kama mkiliamini. Mungu awe pamoja nanyi.

60-0311 Imani Ya Mariamu
Madison Square Garden
Phoenix, Arizona Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org